

Jiunge >>> **WHATSAPP** <<< kwa mafundisho.

Ikiwa wewe bado hujamjua Kristo kabisa/ hujaokoka. Fahamu kuwa ndoto hii inakujuza kuwa Kristo anakuita akuokoe.

Msalaba hufunua wokovu wa Yesu Kristo, tulioupata kwa kifo chake juu ya mti huo.

Waefeso 2:16

*[16]Akawapatanisha wote wawili na Mungu katika mwili mmoja, kwa njia ya msalaba, akiisha kuufisha ule uadui kwa huo msalaba.*

Hivyo fungua moyo wako upokee wokovu huu bure, Kumbuka hakuna uzima wala tumaini, wala, amani, wala raha, wala faraja nje ya Kristo. Ndio maana umeota msalaba kwasababu Kristo anakupenda, hataki uangamie. Ikiwa upo tayari kumpokea leo basi fungua hapa kwa msaada...

>>>> **KUONGOZWA SALA YA TOBA**

Lakini ikiwa tayari umeokoka. Kristo anakutaka kumuangalia yeye zaidi... Kuongeza kiu yako, kwake, na mawazo yako kwake, na hiyo inaambatana na kujikana nafsi.

Luka 9:23-24

*[23]Akawaambia wote, Mtu ye yote akitaka kunifuata, na ajikane mwenyewe, ajitwike msalaba wake kila siku, anifuate.*

*[24]Kwa kuwa mtu atakaye kuiponya nafsi yake ataiangamiza, na mtu atakayeiangamiza nafsi yake kwa ajili yangu ndiye atakayeisalimisha.*

Hivyo kwa ujumla wake ndoto ya msalaba, aidha umeushika au umeubeba, au umeuona, ni ishara ya kumtazama Kristo.

Bwana akubariki

Washirikishe na wengine habari hizi njema kwa kushea

Ikiwa utapenda kupata msaada wa kumpokea Yesu maishani mwako

Kuota msalaba maana yake ni nini?

bure, Basi wasiliana nasi kwa namba uzionazo chini ya makala hii.

Pia kwa kupokea mafundisho ya kila siku kwa njia ya WHATSAPP, jiunge na channel yetu kwa kubofya link hii >>

<https://whatsapp.com/channel/0029VaBVhuA3WHTbKoz8jx10>

Kwa mawasiliano: +255693036618 au +255789001312

Bwana akubariki.

### **Mafundisho mengine:**

*MSALABA NI ZANA YA UJENZI WA MAISHA YAKO.*

*KUOTA UPO MAKABURINI.*

Kuota msalaba maana yake ni nini?

*KUOTA UMEACHWA NA GARI.*

**Rudi Nyumbani**

Share on:  
WhatsApp